JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI (PDPC)

KWA KUSHIRIKIANA NA HILTON LAW GROUP

TAARIFA YA PAMOJA KWA VYOMBO VYA HABARI

WARSHA YA KUONGEZA UELEWA KUHUSU DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

25 Novemba 2024

Dodoma — Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kwa ushirikiano na Kampuni ya Wanasheria ya Hilton Law Group tumeandaa Warsha maalumu ya kuongeza uelewa kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Warsha hii inalenga kuelimisha wadau wa ulinzi wa taarifa binafsi nchini na kutoa elimu pamoja na maarifa muhimu kwa taasisi za umma na binafsi kuhusu kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya 2022 na kanuni zake kuelekea ukomo wa tarehe 31 Disemba 2024, kama ilivyoelekezwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati akizindua Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi alisema kuwa taasisi zote za umma na binafsi ziwe zimejisajili kwenye Tume ya Ulinzi wa Taarifa binafsi kabla au kufikia tarehe hiyo.

Katika mazingira ambayo mageuzi ya kidijitali yameleta mabadiliko makubwa katika maisha yetu ya kila siku, pia yamepelekea kuwepo kwa baadhi ya changamoto. Katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu zinalindwa, warsha hii itakuwa jukwaa muhimu kwa wadau (Wakusanyaji, Wachakataji na Wahusika wa Taarifa) kuzielewa na kuzitekeleza kanuni mpya za ulinzi wa taarifa binafsi na kuhakikisha kuwa wako tayari kulinda taarifa za watu na haki zao za faragha kwa mujibu wa sheria husika. Washiriki watapata maarifa kuhusu mbinu bora za usimamizi wa taarifa, wajibu wa sheria, na umuhimu wa kulinda taarifa binafsi.

Warsha hii itafanyika kuanzia tarehe 17 na 18 Disemba 2024 Jijini Dar es salaam katika ukumbi wa Superdome Masaki. Washiriki wanatakiwa wajisajili kupitia tovuti ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi www.pdpc.go.tz na kuhakikisha wanapata nafasi ya kushiriki warsha hii ukumbini au kwa njia ya mtandao (online). Maafisa ulinzi wa taarifa binafsi (DPOs) wa Taasisi za umma na binafsi wanahimizwa kushiriki kwa kuzingatia unyeti wa nafasi zao. Tume pamoja na Hilton Law Group itatoa gharama nafuu za ushiriki tofauti na wadau wengine kwa kundi hili.

Warsha hii maalumu itakuwa na wataalamu watoa mada kutoka Tume (PDPC), Hilton Law Group na maeneo mengine yenye wabobevu wa masuala ya ulinzi wa taarifa binafsi nchini, ambao watawasilisha mbinu na mikakati muhimu ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika ulinzi wa taarifa binafsi. Washiriki watapata fursa ya kujadili, kuuliza maswali, na kuungana na wenzao (networking) katika safari ya utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na uzingatiaji wa ulinzi wa haki ya faragha nchini hususani tukiwa tunaimarisha uchumi wetu wa kidijitali.

"Warsha hii ni hatua muhimu katika kukuza utamaduni wa ulinzi wa taarifa ndani ya taasisi zetu. Tunawahimiza wadau wote hususani Wakusanyaji na Wachakataji wa Taarifa Binafsi kuhakikisha kwanza wanajisajili kwenye mfumo wa Tume na kuanza kuchukua hatua mapema ili kuhakikisha sote tunatekeleza maagizo ya Mhe. Rais ifikapo mwisho wa mwaka 2024" alisema Dkt. Emmanuel L. Mkilia, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Naye Wakili Msomi Dorothy Ndazi wa Hilton Law Group aliongeza, "Kadri tunavyokaribia tarehe ya mwisho ya kujisajili iliyowekwa na Mheshimiwa Rais, ni muhimu kwa taasisi zote kuelewa wajibu wao kuhusu dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi. Warsha hii itatoa msaada mkubwa katika kuwaongoza Wakusanyaji na Wachakataji wa taarifa binafsi nchini kupitia hatua zinazohitajika ili kukidhi mahitaji ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa binafsi na kanuni zake."

.....Mwisho.....

Maelezo kwa Vyombo Vya Habari:

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na:

Innocent Mungy kupitia innocent.mungy@pdpdc.go.tz au

simu +255767000474

Tunatarajia ushiriki wako katika juhudi hii muhimu ya kuboresha Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini kwetu. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea kurasa zetu za mitandao ya kijamii